

Chanjo ya HPV

Virusi vya Papiloma ya Binadamu (Human Papillomavirus, HPV) ni virusi vinavyoweza kusababisha saratani. Chanjo ya HPV ni muhimu kwa kukinga saratani.

Chanjo ya HPV inakinga maambukizi ya aina mbaya zaidi za virusi vya papiloma. Chanjo hii ni salama na yenye ufanisi na inapendekezwa kwa wavulana na wasichana kuanzia umri wa miaka 11, lakini inaweza kutolewa mapema kama miaka 9.

Chanjo hii inafanya kazi vizuri ikitolewa mwanzoni mwa kipindi cha kubalehe, ili kutoa nafasi ya kinga kuundwa, jambo linalomaanisha kinga bora wakati vijana wanaobalehe wanavyozidi kukua.

Chanjo: Hatua bora kwako katika kujikinga.

Ukiwa na maswali, muulize mto huduma wako wa afya.

**KWA MAELEZO ZAIDI KUHUSU
CHANJO NA MAGONJWA,
TEMBELEA**

- hhs.iowa.gov/public-health/immunization
- www.immunize.org
- www.cdc.gov/vaccines
- www.aap.org

Virusi vya Papiloma vya kibinadamu (Human papillomavirus, HPV)

Chanja kwa maisha bora!



Health and
Human Services
Public Health



Health and
Human Services
Public Health

JE, HPV NI NINI?

HPV huenezwa kwa mgusano wa kingono hata ikiwa mtu aliye na maambukizi hana ishara wala dalili. Katika matukio mengi, HPV huondoka yenyewe na watu walioambukizwa virusi hivi huwa hawajui kuwa walikuwa navyo. Hata hivyo, ikiwa HPV haitaondoka inaweza kusababisha matatizo ya kiafya kama vile vipele vya chunjua kwenye sehemu za siri na saratani. Saratani mara nyingi huchukua miaka kukua baada ya mtu kuambukizwa HPV. HPV inaweza kuwa na matokeo mengi mabaya kwa wanaume na wanawake:

- saratani ya shingo la kizazi
- saratani njia ya uke
- saratani ya uke
- saratani ya njia ya haja kubwa
- saratani ya uume
- saratani ya koo na vipele vya chunjua vya sehemu za siri

UKWELI KUHUSU HPV

- Wamarekani milioni 79 kufikia sasa wameambukizwa HPV
- Watu milioni 14 hupata maambukizi mapya ya HPV kila mwaka
- Watu 36,500 nchini Marekani wanakadiriwa kugunduliwa na saratani inayosababishwa na maambukizi ya HPV
- 90% ya saratani zinazosababishwa na HPV zinaweza kuzuiwa kwa chanjo ya HPV idadi inayokadiriwa kuwa matukio 33,700 kila mwaka nchini Marekani
- Chama cha Saratani Nchini Marekani (The American Cancer Society) kinatarajia matukio mapya ya maambukizi 12,000 ya saratani ya shingo ya kizazi yataokea nchini Marekani na takribani wanawake 4,000 watakuwa kutokana na ugonjwa huu kila mwaka

KUJIKINGA NA HPV

Chanjo ya HPV inatoa manufaa makubwa ya kiafya kwa watu wanaokamilisha huu msururu wa chanjo kabla kupata HPV. Chanjo ya HPV ni salama na yenye ufanisi na inapendekezwa kwa wavulana na wasichana kuanzia umri wa miaka 11, lakini inaweza kutolewa mapema katika umri wa miaka 9. Inapendekezwa kuwapatia chanjo waliyokosa vijana wanaobalehe na watu wazima kiasi.

JE, NI DOZI NGAPI ZA CHANJO YA HPV ZINAHITEJIKA?

Msururu wa chanjo ya HPV unajumuisha dozi mbili au tatu katika kipindi cha miezi 6 na zinaweza kutolewa wakati mmoja na chanjo zingine. Msururu mkamilifu wa chanjo ya HPV ni muhimu kwa kutoa kinga kamilifu. Chanjo hii inafanya vyema katika vijana wanaoanza kubalehe (umri wa miaka 11 hadi 12) na inatoa kinga ya muda mrefu.

JE, CHANJO YA HPV NI SALAMA?

Chanjo nchini Marekani ni salama na zenyе ufanisi. Madhara ya kawaida yanayotokana na chanjo ni madogo na yanajumuisha uchungu kwenye eneo lililodungwa sindano ya chanjo au joto la kiwango cha chini. Dalili hizi ndogo ni za kawaida na zinapaswa kutarajiwa wakati mwili unapotengeneza kinga. Mimenyuko mikali ya mzio ni nadra sana. Yeyote anayepokea chanjo anapaswa kufahamishwa kikamilifu kuhusu manufaa na hatari zake. Maswali au wasiwasi wowote unapaswa kujadiliwa na mtoa huduma wako wa afya.

REKODI ZA KUCHANJWA

Uthibitisho wa kuchanjwa unaweza kuwa na umuhimu katika maisha yote. Zungumza na mtoa huduma wako wa afya kuhusu kuingiza taarifa za kuchanjwa katika Mfumo wa Taarifa wa Rejestra za Chanjo wa Iowa (Iowa's Immunization Registry Information System, IRIS) na kupata nakala ya rekodi zako.

Kote ulimwenguni, saratani ya shingo ya kizazi ni saratani ya **nne kuwapata zaidi wanawake** na inakadiriwa kusababisha zaidi ya matukio mapya 604,000 ya saratani na **vifo 342,000 kila mwaka**.

